**Jiwe La Kiroho la kujengea namba 47.**

***1 Yohana 3:11-12;*** " Maana hii ndiyo habari niliyoisikia tangu mwanzo kwamba tupendane sisi kwa sisi kama kaini alivyokua Yule muovu akamuua ndugu yake naye alimuua kwa sababu gani? Kwa sababu matendo yake yalikua mabaya na ndugu yake yalikua ya haki".

***Methali 30-20;*** Hivyo ndiyo ulivyo muenendo wa mwanamke mzinifu hula akapangusa mdomo wake na kusema hakufanya uovu.

Sasa hiyo ndiyo sababu tunaamini kwamba biblia inatuambia sisi kabla ya dunia kuumbwa na kabla haijaweza kuwepo kwamba baba alimuua mwanakondoo ***(Ufunuo 13-8)*** na halafu alipomuua mwanakondoo aliandika majina ya kila mmoja wa watoto wake ambao walikua wanakuja katika kitabu cha uzima. Tunaishi katika huo wakati mpaka uweze kumalizika wote. Unaona kile ninachomaanisha? Mungu asiye na Mwanzo wala mwisho alijua kwamba kabla ya dunia kuanza aliona ule utaratatibu wa kile ambacho kitaenda kufanyika nae akakifanya hivyo.

Sasa kumbuka yeye kama mjenzi mkuu aliye hodari baba alipoifanya hii dunia na akaweka kalsham patasiam na petriliam na haya madini ya aina mbalimbali ambayo yanaenda kuunda mwili wa mwanadamu alijua mwisho wake wa umilele utakua wapi na alijua aina ya Roho gani itakaa katika mwili tutafuatilia hayo katika uzao wa nyoka na katika uzao wa nyoka na katika uzao wa mwanamke na kuyaleta hapa chini na kuwaonyesha kwanini iko hivyo. Uone vile uzao wa nyoka uliendelea hapa chini na vile ambavyo uzao wa mwanamke uliendelea hapa chini ***(Wafilipi 2:5-8)*** jinsi ule uzao wa nyoka ulivyoanza na kufika mahali na kuweza kutawala ukaweza kukua na kua mkubwa mkubw mpaka sasa hakuna chochote ila kundi dogo tu la mabaki ya majina yaliyoachwa ambayo yameandikwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu ***(Waefeso 1:3-4)*** [1]

Ninyi watu sasa mmeniskia mimi nikihubiri juu ya uzao wa nyoka na hilo haliwezi kukataliwa hilo lilifunuliwa katika moja ya hii mihuri saba ilikua imefichika ***(Ufunuo 10:1-7)*** ulipaswa kuje chukua ni lazima kuje Mungu alikusudia hivyo kwamba utakuja hivyo mihuri saba lazima ifunguliwe ***(Ufunuo 5:1-7)*** ilikua hakuna shaka yoyote juu ya hiyo………………siyo kama vile tunavyolisifu hatuna la kujisifia ni bwana Yesu Kristo tu hakuna hata mmoja wetu

***(2 Wakorintho 10:17-18)*** sisi tunamsifu hatuna la kulisifia ni bwana Yesu Kristo tu hakuna hata mmoja wetu ***(2 Wakorintho 10:-17-18)*** sisi tunamsifia tu bwana Yesu sasa kumbuka motto wa shetani alikua kaini ***(1 Yohana 3:11-12)*** hawa alipata mimba kwa shetani na katika siku ile ***(Mwanzo 3:1-7)*** kwahiyo shetani asubuhi ile pengine alikutana na huyu muovu ambae alikua ni Nyoka siyo Mjusi lakini alikua ni Mnyama Mwerevu sana mwenye akili hodari kuliko wanyama wote walikuwepo wakiwa chini ya mwanadamu na mwanadamu mwenyewe ni mnyama na sisi ni wanyama wanyeshao wenye damu ya moto wanyama huyu nyoka alikua ndiye mnyama anaemfuatia mwanadamu alikua anasimama kati ya mwanadamu na sokwe mtu sasa wanasayansi wanatafuta huyo mnyama anaekosekana kati ya mwanadamu na sokwe mtu (Kiungo kinachokesakana) na hiyo imefichika sana kwa kumuweka chini kabisa hakuna hata mfupa ndani yake unaofanana na wa mwandamu kumfanya yeye awe mjusi mnyama mwenye damu baridi . [2]

Unaona hawawezi kupata aina hiyo ya mnyama uliyo kati ya sokwe mtu na mwanadamu unaona kila mmoja jinsi ilivyoendelea mbele kutoka ndege kuendelea mbele mpaka manyani nakadhalika mpaka kufikia sokwe mtu halafu hapo wanapotea anaekosekana hapo (sepent) ni nyoka siyo nyoka mjusi kila umbile lake limepotea kutoka kwake kwa sababu yeye akilaaniwa ***(Mwanzo 3:14).*** [3]

Sasa tuona kwamba huyu nyoka alimkuta hawa pale bustani ya edeni na huyu msichana mdogo ambaye hakujua dhambi hakujua hali ya uchi wake ulivyokuwa na yeye nyoka alijua alikua mwerevu mjanja mwenye hekima na akwamwambia huyu mwanamke " Ile mbegu, lile tunda lilikua tamu na linatamika na alipokaa nae asubuhi ile ***(Mwanzo 3:-7)*** na halafu unaona hapo sasa mchana wake yule mwanamke alimshawishi adamu afanye jambo lile lile akimwambia vile lilivyokua nae adamu kwa makusudi kabisa akijua kwamba hapaswi kufanya hivyo alitembea na mkewe na kufanya jambo hilo ambalo kwa vyovyote hatimaye angelifikia lakini unaona ilipaswa iwe hivyo hekima ya Mungu ***(1 Wakorintho 2:6-8)*** kwasababu ya hili sasa lina dhihirisha sifa ya Mungu kua mkombozi , baba mponyaji.

Yeye alikuwa cha wenyewe kule nje katika uhuru wa kuamua akiwaacha watende asingelifanya walitende hilo naye abakie kua mwenye haki lakini aliweza kuwafanya wawe sawa na yeye na kuwaacha wao walifanye hilo wenyewe na yeye alijua kwamba wangelifanya hilo kwahiyo sasa unaona adamu alipoishi nae

alienda kuzaa mapacha na mmoja wapo alikua ni wa shetani na mwingine alikua ni wa adamu ambae alikua ni wa Mungu. Kaini na habil ***(Mwanzo 4:1-2)*** tunalo tukio sasa kule takson mwanamke wa kizungu aliyeishi na mumewe asubuhi ile na mchana wake aliishi na mwanamke mweusi alafu watoto wawili mapacha wakazaliwa mmoja wao alionekana na kichwa kama muamerika mweusi na mwingine alionekana na kichwa kama ni mzungu naye alikua anajaribu kumfanya yule baba wa kizungu awatunze watoto wote naye akasema mimi nitamtunza wa kwangu na siyo wa huyo mwingine muache huyu muamerika mweusi atunze mtoto wake unoana jambo hilo ni kweli siku zote kuna mapacha itakua karibu sana (vinafanana) kiasi cha kuweza kumdanganya mteule. Unaona litaenda kuwadanganya wao kwa sababu linaonekana kama ni kitu kile kile unaona? Lakini moja wapo hapo ambapo neno linaangukia lakini moja wapo kama ilivyo hapa imetoka unaelewa? Unaona moja wapo imetoka kwa sababu ni baba asiye sahihi ambayo naweza kuthibitisha siku moja kama Mungu ataniruhusu mimi kwamba madhehebu haya ni chapa ya mnyama unaona ni baba asiye sahau yeye anawachanganya watu kuelekea kwenye mambo ya kidhehebu badala ya neno la Mungu unaona ni baba asiye sahihi ni uamsho wa kaini ninapoenda nyumbani wakati huu ninaenda kuhubiri juu ya somo ule mkondo wa nyoka yule mnyama pale mwamzo na yule mnyama pale mwishoni ***(Ufunuo 13:15)*** na tutaenda kumfuatilia yeye kupitia kwenye biblia na kuonyesha jinsi ambavyo anakuja sasa na halafu uone vile alivyo mwerevu sana yeye yuko hasa kama………..vema wako kama Yuda na Yesu pale wote esau na Yakobo na kama vile kunguru na njiwa wakiwa wote katika kiota kimoja au safina na kila kitu ni mapacha katika huo mfumo mkuu ambao tunaishi ndani yake yule adui anatumia udanganyifu kama alivyofanya kwa hawa " oh Mungu amesema ? hakika lakini hakika" Unoana? Kujaribu kuweka hoja zaidi ya Mungu alichokisema pale mwamzoni " Hakika utakufa" ***(Mwanzo 3:1-7).***

Alisema " ndiyo Mungu alisema hivyo lakini hakika……………. " unaona vile alivyompulizia hilo unaona lakini kile Mungu anachosema Mungu anakisimamia hicho. Kwahiyo kamwe usijaribu kudanganywa na hilo sasa tunaona kwamba hiyo ilizaa kwa jinsi yake sasa katika mwanzo hapa unaona kwamba baada ya kupuliziwa ile sumu ya maarifa hebu tuchukue mwanzo sura ya 4:16 kaini akatoka mbele ya uso wa Bwana sasa angalia jambo la kwanza alilolifanya unaona kaini akatoka mbele za uso wa bwana hapo alifanya kosa lake na hapo ndipo ninaweza

kufanya kosa ni dakika ile nitakapoondoka kutoka uweponi pa bwana sasa angalia mara tu walipoondoka kutoka uweponi pa bwana walianza kujenga miji walianza kutengeneza vyombo walianza mambo ya sayansi na kutengeneza vitu vya shaba na kupiga muziki nakadhalika. (***Mwanzo 4:17-22)*** unaona? Sasa hiyo inatoka wapi? Nani alitoka nje? Kaini Yule wa Nyoka unalielewa hiko kaini alindoka akatoka na uangalie aliondoka kutoka uweponi pa bwana akaanza kufanya vitu vya kisayansi sasa angalia yeye anachofanya unaona sayansi, elimu, miji,ustaarabu vyote ni vya shetani nani alianzisha hayo? Shetani mambo hayo ni ya nani leo? Ya shetani mabomu ya atomiki na matumbo kama haya alianzisha haya ? Shetani tunaishi katika hali hiyo tunapaswa kuishi hapa sisi ni viumbe tunapaswa kukaa hapa. Lakini ustaarabu mkuu wa Mungu hautakua na kitu chochote kama hicho unaona? Sayansi inachukua viti vya asili na kuvipotosha kwa kufanya vitu ambavyo hakikukusidiwa kufanya.

Kaini alijua mapenzi makamilifu ya Mungu kaini alijua haya kwanini? Lakini alikataa kufanya hayo na alithibitisha kwamba yeye ni uzao wa Nyoka pale alipoona mapenzi makamilifu ya Mungu alipokataa kufanya hayo alimuona Mungu akaudhibitisha ujumbe wa habil naye alijua kwamba hayo ni mapenzi ya Mungu unaona? Alimuona Mungu akithibitisha ujumbe wa habil na Mungu akamwambia nini? Yeye alimuambia fanya hivyo kama ndugu yako fanya ibada kama ndugu yako na utafanya vyema aliona mapenzi makamilifu ya Mungu lakini hakuyataka hayo unaona alitaka kuongeza kitu flani katika hilo. ***(Mwanzo 4:1-7)***

Na hawa wanatheolojia wanaiona hii biblia mpya wanasoma hiyo lakini hawataki kufanya vile inavyosema unaona inaonyesha ni uzao wa Nyoka wameliona hilo likithibitishwa na kirahisi sana machoni pa watu lakini wamekana kwamba ni vigumu mno kwa watu kukubali kujinyenyekeza wenyewe katika neno la Mungu ***(Yakobo 4:6).***

Angalia vile kaini alivyofanya hakuweza kujinyenyekeza mwenyewe kwa neno lile la Mungu likidhibitishwa hangeweza kufanya hivyo kama siyo dhambi inakuotea mlangoni kutokuamini huko pale halafu akafika mahali aliposhindwa kutii kwa makusudi na ukijua kufanya jambo jema na usilifanye kwako ni dhambi kama unajua kitu ambacho ni sahihi na usikifanye ***(Yakobo 4:17)*** unaona hapo sasa akawa ambae alishindwa kutii kwa makundi baada ya neno limedhihirishwa kwake hapo sasa akavuka mstari wa utenganisho alipovuka alitolewa edeni kuna mstari

ambao unaenda kwa umbali flani na ukaenda umbali zaidi na kuvuka unakwenda upande mwingine umetoka nje unajua hilo unaelewa hilo hakuna mstari kama huamini hilo soma ***(Waebrania 10:26)*** huo ndio mstari ambao nilikua ninaunyaka. [2].

Sasa Mungu hakumlaani adamu angeweza kufanya jambo hilo hilo lakini alilaani dunia mbigili na miiba ***(Mwanza 3:17-19)*** hakumlaani hawa lakini alisema Adamu atakua Mtawala wake alimuambia Adamu atakua Mtawala wako ***(Mwanzo 3:17)*** kwanzia sasa na kuendelea hatakiwi ajaribu kuhubiri au chochote
***(Wakorintho 14:34-35)*** Adamu ni Mtawala wake " na siku zote za maisha yako na kwa Uchungu utaleta uhai katika dunia" lakini alisema nitaweka uadui kati ya uzao wako ***(Mwanzo 3:15)*** sasa yeye mwanamke hakua na mbegu yoyote kamwe hakua nayo kwa hiyo ilibidi apokee mbegu kutoka mahali Fulani Mungu akampa yeye Mbegu kutoka mahali Fulani Mungu akampa yeye Mbegu siyo kwa kujuana kimwili bali kwa kuumba.
Enyi watu vipofu hamuwezi kuona hilo uzao wa Nyoka? Oh jamani Shetani alifika pale kabla ya adamu hiyo ndiyo ilikua mbegu lakini alipokea mbegu
***(Luka 1:26-33)*** ***(Isaya 7:14)*** ilikua ni mwanzo wa kuumba wa Mungu [3].

Nami nilikua ndani ya Kristo na wewe ulikua ndani ya kristo kabla ua kuwekwa misingi ya Dunia ***(Waefeso 1:3-4)*** alikuja kuokoa walio wake walio wake ambao walikua ndani yake (Halleluya) watoto wake walio kuwa ndani yake
***( Yohana 17:6-8)*** kamwe hakuja kuokoa watoto wa Shetani ***(Yohana 17:9), Mathayo 13:36-39)*** kamwe hawatalijua hilo nao ni wajanja mno katika njia zao za kiakili za kusoma kiasi kwamba hawezi wakalinganishwa na wao hata kidogo huwezi ukaswashinda katika kuzungumza lakini kwa imani unaliona hilo. [4].

**<u>NUKUU ZA KINGEREZA.</u>**

1. Ubatizo wa Roho Mtakatifu (58-0928M) aya 76-78
2. Nguvu ya kugeuzwa (65-1031M) aya 123-139,144-148,246-249,254
3. Makao ya baadae (64-0802) aya 325,326-330
4. Nawe hujui (65-0815), aya 137-138
5. 

---

6. Jiwe la kiroho la kujengea No. 47 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
7. Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
8. www.biblebelievers, Fax(+49)72353306

---

9. Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
10. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

11. *Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
12. *Charles E. Y. Kanju,*
13. *Box 553 Korogwe -  Tanga*
14. *E-mail: Chaelika@livel.com*
15. *Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*